Mzee Wassira atinga Dodoma na baraka za Baba wa Taifa ..Uk.4

Mitandao @JAMVILAHABARI Jamvi la habari jamvihabari +255676807684 Email: jamvinews@gmail.com

GAZETI LAKO

# JAMVI LA HABARI

ISSN Na 2683 - 6548: Toleo Na. 2519 JUMATANO FEBRUARI 05, 2024 Bei Tsh. 1000 Kenya Ksh. 60 www.jamvilahabari.co.tz

# DKT SAMIA ATUNUKIWA TUZO YA AFYA YA KIMATAIFA

>> **Ni** kutokana na juhudi za Serikali kupunguza vifo vya mama na mtoto

>> **Naye** airudisha kwa wauguzi wa afya wa kada zote nchini

Uk.2




*Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan akipokea Tuzo Maalum ya Kimataifa ya The Global Goalkeeper Award kutoka kwa Rais wa Kitengo cha Usawa wa Jinsia kutoka Taasisi ya Gates, Dkt. Anita Zaidi kwenye hafla iliyofanyika katika Hoteli ya Hyatt Regency Jijini Dar es Salaam tarehe 04 Februari, 2025*

# Leo ndio leo Dodoma

>> **Wana** CCM wafurika kuwalaki Dkt. Samia, Dkt. Mwinyi na Dkt. Nchimbi

>> **Macho** na masikio vyaelekezwa Uwanja wa Jamhuri katika jambo zito

>> **Kila** kona ya Tanzania ni sherehe kubwa kuadhimisha miaka 48 ya CCM Uk.2

## Neno la Dkt. Samia lasubiriwa kwa hamu

Uk.3

# DKT SAMIA ATUNUKIWA TUZO YA AFYA YA KIMATAIFA

NA MWANDISHI WETU

RAIS wa Jamhuri wa Muungano wa Tanzania Dkt. Samia Suluhu Hassan amepokea Tuzo ya 'The Gates Goalkeepers Award' ikiwa ni kielelezo cha matokeo makubwa yaliyopatikana katika uongozi wake kufuatia ripoti ya utafiti wa Demokrasia na afya ya mwaka 2022 inayoonyesha kupungua kwa vifo vitokanavyo na uzazi kwa asilimia 80.

Dkt Rais Samia ndiye kiongozi wa kwanza kupokea tuzo hiyo kwa Bara la Afrika jambo lililochochewa na uongozi wake mahiri ulioleta mafanikio makubwa nchini hususani katika sekta ya afya kwa kuitendea haki na kusababisha mataifa makubwa duniani kuutambua mchango wake.

Amesema mafanikio haya yametokana na mikakati mbalimbali iliyotekelezwa na inayoendelea kutekelezwa kutokana na utashi wa kisiasa chini ya uongozi wa Rais Dkt. Samia kuweka mazingira wezeshi kisera pamoja na kuimarisha rufaa za akina mama na watoto.

Dkt Samia alikabidhiwa tuzo hiyo maalum ya Kimataifa 'The Global Goalkeeper Award' imetolewa kutoka kwa Rais wa Kitengo cha Usawa wa Jinsia, Taasisi ya Gates, Dk Anita Zaidi katika hafla iliyofanyika katika Hoteli ya Hyatt Regency Jijini Dar es Salaam

Dkt. Zaidi alisema usimamizi wa afya ya uzazi na lishe ni miongoni mwa sababu zilizompa Rais Dkt Samia Suluhu Hassan tuzo hiyo ya Gates Goalkeepers.

Akizungumza katika Uwanja wa Ndege jijini Dodoma muda mfupi baada ya kuwasili, Rais |Samia alisema licha ya yeye kupokea heshima hiyo lakini naye anaikabidhi kwa wauguzi wa kada mbalimbali ambao ndiyo wanaohusika zaidi katika utekelezaji wa majukumu haya.

Alisema juhudi hizo kwa pamoja zimewezesha kupunguza vifo vya mama na mtoto kwa asilimia 80 huku juhudi zikiwekezwa zaidi ili iweze kupungua zaidi, hii ikitokana na uwekezaji wa serikali katika ujenzi wa zahanati, vifaa tiba pamoja na madawa na uwezeshaji mwingine katika sekta ya afya.

Dkt Samia alipokewa jijini Dodoma na Katibu Mkuu wa Chama cha Mapinduzi, (CCM) Dkt. Emmanuel Nchimbi pamoja na viongozi wengine wa chama hicho pamoja na wale wa serikali.

Leo Rais Dkt. Samia anatarajiwa kuwa mgeni rasmi katika sherehe za CCM kutimiza miaka 48, zitakazofanyika katika Uwanja wa Jamhuri jijini Dodoma.




# MZEE WASSIRA ATINGA DODOMA NA BARAKA ZA BABA WA TAIFA

NA MWANDISHI WETU, DODOMA

MAKAMU Mwenyekiti wa Chama cha Mapinduzi (CCM), Mzee Steven Wassira ni miongoni mwa wenyeji katika sherehe za chama hicho kutimiza miaka 48, ambaye ameingia jijini Dodoma akitokea Butiama mkoani Mara ambako alitembelea kaburi la Rais wa Kwanza wa Tanzania Hayati Mwalimu Julius Kambarege Nyerere.

Mzee Wassira alikwenda kuzuru kaburi hilo la Baba wa Taifa baada ya kufanya mkutano mkubwa mjini Bunda, ikiwa ni maandalizi ya kuelekea sherehe za kuzaliwa CCM zinazofikia kilele hii leo.

Katika mkutano wa Bunda na ule wa mjini Geita, Mzee Wassira aliwataka Wananchi na wana CCM kuendelea kukiamini chama hicho kutokana na kazi kubwa iliyofanywa, pia akiwataka wapuuze maneno ya kukatisha tamaa yanayotolewa na wapinzani.

Katika ziara hizo za kwanza tangu aliposhika wadhifa huo Mzee Wassira, alionekana kukubalika kutokana na uchambuzi wake makini wa sera za CCM, pia akitoa ushahidi wa utekelezaji wa Ilani ya CCM.

Wassira alisema katika Utawala wa Awamu ya Sita chini ya Utawala wa Dkt Samia, CCM haina haja ya kutangaza mafanikio ya utekelezaji wa Ilani kwa vile kila kona ya Tanzania maendeleo yanajipambanua.

Mwanasiasa huyo mkongwe leo anatazamiwa kuunguruma kutokana na itifaki, kabla ya wananchi kusikia maneno ya makada wao waliopewa ridhaa ya kupeperusha bendera ya CCM kuwania nafasi za juu, Urais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mgombea Mwenza pamoja na Rais wa Zanzibar.

# LEO NDIO LEO DODOMA

NA MWANDISHI WETU

LEO ndio leo, unaweza kusema hivyo kutokana na Jiji la Dodoma kufurika idadi kubwa ya wageni hususan Wana CCM waliofika kwa ajili ya kuhudhuria sherehe za chama hicho kutimiza miaka 48.

CCM ilizaliwa Februari 2, 1977 ambapo sasa kimefikisha umri huo, huku kikiwa na mafanikio makubwa ya kujivunia, ikiwemo ya kuongoza nchi kwa kipindi chote cha umri wake.

Katika sherehe za leo yapo mambo mengi yameoandaliwa lakini kubwa ni kutambulishwa kwa Makada wa CCM waliopewa dhamana ya kugombea nafasi ya Urais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Zanzibar na pia Mgombea Mwenza atakayepeperusha bendera sambamba na mgombea wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Wana CCM hao ambao leo watatambulishwa rasmi kwa wanachama wao, ni Dkt Samia Suluhu Hassan ambaye pia ni mwenyekiti wa chama hicho na Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Dkt Hussein Mwinyi, Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi na Rais wa Zanzibar atakayegombea upande wa Zanzibar na Dkt. Emmanuel Nchimbi, Katibu Mkuu wa CCM ambaye ameteuliwa kuwa mgombea mwenza wa Dkt Samia Suluhu Hassan.

Maandalizi ya sherehe hizo yalianza muda mrefu lakini jana Katibu wa Itikadi, Uenezi na Mafunzo wa CCM, Amos Makalla aliwaambia waandishi wa habari katika mkutano uliofanyika jijini Dodoma kuwa, katika sherehe hizo pia CCM itawatambulisha wagombea wake hao.

Makalla alikisifu chama hicho kuwa na mtaji mkubwa wa wanachama wanaofiukia milioni 12, pia kikiwa na ridhaa ya muda mrefu ya kuiongoza nchi, hivyo aliwataka wana CCM na Wapenzi wa chama hicho kujivunia mafanikio hayo.

# Waiomba Serikali kuorodhesha maporomoko

NA MWANDISHI WETU, KALAMBO, RUKWA

SERIKALI imeombwa kuorodhesha maporomoko ya maji ya Kalambo (Kalambo Water-Falls) mkoani Rukwa kwenye orodha ya urithi wa Dunia wa UNESCO ili kuchagiza utalii na kutengeneza fursa za ajira kwa vijana na wanawake mkoani humo.

Wito huo umetolewa wilayani Kalambo Januari 30,2025 na Mkurugenzi wa TAMCODE Bi. Rose Ngunangwa wakati wa ziara ya shirika hilo pamoja na waandishi wa habari iliyofanywa kwa ufadhili wa UNESCO- Alwalweed Philanthropies.

Maporomoko hayo ya kipekee yana urefu wa mita 235 (futi 772) na ni ya pili Afrika ambapo pia yamezungukwa na misitu na uoto wa asili ikiwemo hewa safi.

Bi. Ngunangwa amesema kuorodhesha kwenye urithi wa dunia wa UNESCO kutasaidia maporomoko hayo kujulikana dunia nzima na kuchochea wawekezaji na utalii na nchi kutengeneza fursa za ajira kwa wanawake na vijana mkoani Rukwa na kuongeza pato la taifa.

Vilevile, Bi, Ngunangwa ameiomba Wizara ya Utalii na Maliasili kuchagiza wawekezaji kutoka katika sekta ya umma na binafsi ili wajenge mahoteli na kutoa huduma za chakula na huduma nyingine za kibinadamu.

Kwa upande wake, Afisa Michezo na Utamaduni wa Mkoa wa Rukwa, Adam Evarist amesema kwamba hapo awali ilikuwa ngumu kidogo kuweza kuona asilimia mia moja ya maporomoko hayo kutokana na miundombinu lakini kwa sasa serikali imejenga ngazi 1270 zinazoshuka hadi chini.

Evarist amesisitiza umuhimu wa kuendelea kutunza misitu ili urithi huo urithishwe kwenye vizazi vijavyo.

Ziara hiyo imewajumuisha waandishi wa redio na runinga za kidigitali mkoani Rukwa na Katavi, watendaji wa TAMCODE, pamoja na Afisa Utamaduni wa Manispaa ya Sumbawanga ili kuchagiza umuhimu wa kutunza misitu, utalii na urithishwaji wa utamaduni usioshikika na unaoshikika.

# Serikali yaagiza wananchi kulindwa dhidi ya wanyama pori

NA MWANDISHI WETU

WAZIRI wa Maliasili na Utalii, Mhe. Balozi, Dkt. Pindi Chana (Mb) amezielekeza halmashauri zote nchini kuchukua jukumu la kulinda wananchi dhidi ya wanyamapori wakali na waharibifu kwa kushirikiana na Wizara ya Maliasili na Utalii na taasisi zake.

Ameyasema hayo Februari 4,2025 Bungeni jijini Dodoma alipokuwa akitoa ufafanuzi kuhusu swali la Mhe. Mhandisi Ezra John Chiwelesa aliyetaka kujua serikali ina mpango gani wa kuondoa adha ya uvamizi wa tembo katika Kijiji cha Nyabugombe Kata ya Nyakahura – Biharamulo.

"Katika bajeti za halmashauri asilimia 10 za mapato ya ndani na kuna maeneo Wizara ya Maliasili na Utalii inarudisha fedha za Wildlife Management Areas asilimia 25, fedha hizi zinatakiwa zitumike kwa shughuli rafiki za uhifadhi kulinda wananchi wasiumizwe," alisisitiza Mhe. Chana.



Amesema ajenda ya kulinda wananchi dhidi ya changamoto mbalimbali ikiwemo za wanyamapori wakali na waharibifu ni ajenda ya halmashauri husika na kusisitiza kwamba zina uwezo wa kununua ndege nyuki 'drones', kusomesha vijana kozi za uhifadhi ili wawe maaskari wa vijiji na kujua namna ya kuwalinda wananchi.

Awali akijibu swali hilo, Naibu Waziri wa Maliasili na Utalii, Mhe. Dunstan Kitandula (Mb) alifafanua kuwa serikali inaendelea kutekeleza mikakati mbalimbali ya kukabiliana na adha ya wanyamapori wakali na waharibifu wakiwemo tembo katika maeneo yanayopakana na Hifadhi ya Taifa Burigi – Chato.

"Mikakati inayotekelezwa ni pamoja na: kuendelea kushirikiana na wananchi kuwadhibiti tembo kwa wakati ambapo jumla ya askari sita (6) wa uhifadhi kwa kushirikiana na mgambo sita (6) wamepewa mafunzo kuhusu tabia za wanyamapori wanatumika kuwafukuza tembo kupitia kituo cha Nyungwe kilichopo Kijiji cha Nyabugombe, Kata ya Nyakahura" alisema Mhe. Kitandula.

Kijiji cha Nyabugombe kilichopo katika Kata ya Nyakahura, ni miongoni mwa vijiji 38 vinavyopakana na Hifadhi ya Taifa Burigi-Chato. Kwa kipindi cha miezi sita Julai – Disemba, 2024 Jumla ya matukio 16 ya tembo yaliripotiwa na kudhibitiwa katika Kijiji cha Nyabugombe kilichopo Kata ya Nyakahura, Wilaya ya Biharamulo.

# DKT SAMIA AHIMIZA UTOAJI HAKI NCHINI



NA MWANDISHI WETU

RAIS Samia Suluhu Hassan amesema ni muhimu kuimarisha utoaji haki ili nchi ipate manufaa katika utekelezaji wa Dira ya Taifa ya Maendeleo 2050.

Rais Samia amesema hayo Dodoma wakati wa maadhimisho ya Siku ya Sheria kuashiria mwanzo wa mwaka wa Mahakama.

Amesema utekelezaji wa Dira ya 2050 hautakuwa rahisi, hivyo ni vyema Mahakama na wadau waanze kujipanga.

Rais Samia alisema katika dira mpya sauti za wananchi wengi zinatamani miaka 25 ijayo Tanzania iwe ni taifa

jumuishi lenye ustawi, haki na linalojitegemea.

Alisema Dira ya 2050 itaweka lengo la kuongeza pato la Taifa hadi kufikia dola bilioni 700 ifikapo mwaka 2050 na ili kufikia hilo ni lazima kuchukua hatua ya kukuza sekta za kiuchumi ikiwemo kuvutia uwekezaji na biashara, kuvutia mitaji nchini na kukuza njia za ukusanyaji wa mapato nchini.

"Kufanya biashara ili kukuza uchumi mambo hayo yote yatalazimu sekta zinazohusika na haki madai kujiandaa vyema katika kutoa huduma za haki," alisema Rais Samia.

Alisema kuongezeka kwa shughuli nyingi za kibiashara na uwekezaji zitazusha migogoro ya kisheria na uhitaji mkubwa wa huduma za utoaji wa haki. "Haitarajiwi kwa wadau na mahakama kutumika kuchelewesha haki na badala yake tunategemea mahakama kuwa mwezeshaji wa shughuli za kiuchumi na kutenda haki kwa haraka na wakati," alisema Rais Samia.

Aliagiza waliopewa dhamana kwenye baraza la ushauri wa kodi kuhakikisha haki inatendeka kwa wakati ili wawekezaji wasicheleweshewe haki na kodi stahiki zilipwe kwa wakati.

Rais Samia alisema miaka 25 ijayo sekta ya fedha itapunguza matumizi ya fedha taslimu mkononi na kuwa na mifumo ya fedha za mitandaoni.

"Kutokana na haya ni lazima tujipange na watu wetu wanaohusika na mambo ya sheria kuangalia mambo haya, lazima tujipange vizuri," alisema.

Rais Samia alisema kikatiba ofisi yenye dhamana na upekuzi na tathmini ya mikataba inayoingiwa na serikali na mashirika yake ni Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali.

Alisema katika kuhakikisha maslahi ya nchi yanaendelea kuzingatiwa kwenye mikataba itakayoingiwa ni lazima watumishi kwenye Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali wawe na uwezo na ubobevu kwenye masharti ya kimikataba yanayohusu sekta za kiuchumi na uwezo wa kusimamia mikataba hiyo.



Rais Samia alisema utekelezaji wa Dira inayoishia 2025 umekuwa na matokeo chanya katika maisha ya wananchi na mabadiliko yako dhahiri katika sekta za kiuchumi, maendeleo ya jamii, sekta ya kifedha na katika sekta ya utoaji haki

na kuwepo kwa maendeleo kwenye miundombinu, vifaa na watumishi.

"Katika mahakama za Tanzania kusikilizwa kwa mashauri ama kutoa ushahidi kwa njia ya mtandao sasa ni jambo la kawaida leo hii sio simulizi tena, tulidhani haiwezekani lakini imewezekana," alisema.

Rais Samia alisema mwaka 2024 mashauri 172,301 yalisajiliwa na kumalizika kupitia mfumo wa mtandao katika mahakama za mwanzo, mashauri 70,714 kwa ngazi ya mahakama za wilaya hadi mahakama kuu.

Alisema maboresho na mageuzi katika Mahakama ni matokeo ya mipango na hatua madhubuti kwenye mpango wa tatu wa maendeleo wa miaka mitano unaoishia mwaka 2025.

Rais Samia alisema Ilani ya uchaguzi ya CCM imeelekeza kuimarisha Tume ya Utumishi wa Mahakama ili iweze kusimamia kwa ufanisi maadili na nidhamu katika utumishi wa mahakama.

Aidha, alisema serikali inatambua mazingira magumu ambayo watumishi wa mahakama wamekuwa wakiyafanyia kazi na akasema ni wajibu wa serikali kutengeneza mazingira mazuri na vivutio kwa watendaji wa mhimili huo.

Rais Samia alisema maombi ya kuboresha maslahi ya watumishi yanaendelea kufanyiwa kazi hatua kwa hatua na jinsi ya hali ya uchumi unavyoruhusu na akasema serikali itaendelea kuangalia maslahi ya sekta hiyo.

Aliwakumbusha majaji na mahakimu wasiwe Mungu watu, wawe upande wa haki na watende haki.

"Kuwa jaji au hakimu ni dhamana ambayo inataka uadilifu na nidhamu isitiliwe shaka hata kidogo. Kazi ya kutoa haki ni kazi ya Mwenyezi Mungu, ambaye pia ana kudra na anajalaa," alisema Rais Samia.

Aliongeza: "Majaji na mahakimu ni mawakala wa utoaji haki hapa duniani lakini mmenyimwa kudra na jalaa, hivyo niwasihi sana, niwaombe sana tusiwe Mungu watu, tutoe haki kwa misingi ya katiba na sheria."

# NENO LA DKT. SAMIA LASUBIRIWA KWA HAMU

NA MWANDISHI WETU



WAKATI Jiji la Dodoma likiwa limehemewa kwa idadi kubwa ya wageni na wenyeji walioingia kwa ajili ya kushuhudia sherehe za CCM kutimiza miaka 48, hamu kubwa ya wananchi wengi ni kumuona Mgombea Urais wa chama hicho ambaye pia ni Rais kipenzi cha Watanzania Dkt Samia Suluhu Hassan.

Wananchi waliozungumza na gazeti hili jana kwa nyakati mtofauti jijini hapa wengi walieleza nia yao ya kutaka kuwaona wagombea wote wa CCM, lakini pia Dkt Samia ambaye kama ndiye 'Nyota wa Mchezo' kwao.

"Natamani nimuone na kumsikiliza Rais wetu kipenzi Dkt Samia Suluhu Hassan, kuna mengi mazuri ametufanyia wakazi wa Dodoma," alisema mchuuzi wa mbogamboga katika Soko Kuu la Dodoma huku akiungwa mkono na wafanyabiashara wenzake.

Licha ya kutaka kumshuhudia kiongozi huyo aliyerejesha tabasamu kwa wananchi katika kipindi chake cha utawala Awamu wa sita, pia wananchi wanataka kuwashuhudia na kuwasikiliza wagombea wengine Dkt Emmanuel Nchimbi aliyeteuliwa kuwa Mgombea Mwenza wa Urais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na pia Dkt Hussein Ali Mwinyi ambaye atapeperusha bendera ya CCM kugombea Urais kwa kipindi cha Awamu ya Nane Kisiwani Zanzibar, pamoja na makada wengine wa chama hicho.


# TANGAZA NASI SASA

*Unatamani kukuza biashara yako kutoka hapo ilipo kuwa kubwa na yenye mantiki zaidi?*

- *Unatamani kuongeza kipato, uelewa na upana wa shughuli zako za kila siku?*
- *Je unataka kuwafikia wateja wako ndani na nje ya nchi kwa kiasi kikubwa ili kukuza biashara na huduma yako?*
- *Fahamu kwamba JAMVI LA HABARI na mitandao yake ya kijamii kama Youtube, Instagram, Facebook, Website na Twitter hutembelewa na maelfu ya wasomaji kila siku Duniani kote.*
- *Hivi unafahamu kuwa JAMVILAHABARI kwa sasa ni moja kati ya Media chache zinazo ongoza kwa kutoa taarifa sahihi na kwa wakati zinazotokea nchini na Duniani kwa ujumla?*

*TANGAZA SASA NA JAMVI LA HABARI KWA PUNGUZO KUBWA LA BEI UPATE MATOKEO YA HARAKA.*

*Kwa matangazo yote kama vile minada, kupotelewa kwa vyeti vya shule, matangazo ya makampuni, nafasi za kazi, zabuni za kazi, maonyesho, dawa za asili, taasisi za elimu, taasisi za dini na mengine mbalimbali mbali mbali.*

*Ni rahisi sana, wasiliana nasi kupitia Whatsap namba +255659555744 au tupigie katika +255743777778 au +255659555744 GHARAMA ZETU NISAWA NA BUREE JAMVILAHABARI; TUMECHAGUA KUKUHUDUMIA www.jamvilahabari.co.tz*

# TANZANIA YAPIGA HATUA TIBA YA KITEKNOLOJIA

NA MWANDISHI WETU

WIZARA ya Afya inaendelea kupiga hatua katika masuala ya teknolojia, ukiwa ni mkakati wa serikali kuhakikisha Tanzania inapiga hatua katika kutoa tiba za kibingwa na kuwa na uwezo wa kutosha kukabiliana na maradhi ya aina yoyote na kuyapatia ufumbuzi ndani ya nchi.

Hivi karibuni Mkurugenzi Mtendaji wa Hospitali ya Taifa Muhimbili (MNH), Prof. Mohamed Janabi, amesema hospitali hiyo, inatarajia kuja na kifaa cha kisasa cha kupima ugonjwa wa kisukari kwa njia ya mate.

Amesema kutokana na kukua kwa matumzi ya vifaatiba vya kiteknolojia duniani, hospitali hiyo yenye hadhi ya kitaifa na kimataifa ni matarajio kuwa na aina tofauti za utaalamu wa hali ya juu na kisasa.

Prof. Janabi, aliyasema hayo mwishoni mwa wiki, muda mfupi baada ya MNH kukabidhiwa vifaatiba mbalimbali, vyenye thamani ya Sh. milioni 125, ikiwamo maalumu kwa ajili ya kukuza uoni wa mishipa ya damu na fahamu wakati wa upasuaji.

Vifaa hivyo vilikabidhiwa na Balozi wa China nchini, Chen Mingjian, kwa Waziri wa Afya, Jenista Mhagama, hospitalini hapo, kwa niaba ya Serikali ya Watu wa China, jijini Dar es Salaam.

"Tutakapokuwa tayari tututaarifu umma kupitia nyinyi waandishi wa hbari. Tutakuwa na kifaa kipya cha kupima kisukari kwa njia ya mate," alisema Prof. Janabi.

Kwa mujibu wa wataalamu wa afya, ugonjwa wa kisukari ni ugonjwa sugu ambao mtu yeyote anaweza kuugua. Inakadiriwa kuwa watu milioni 422 wanaishi na ugonjwa wa kisukari duniani kote, ikiwa ni mara nne zaidi ya miaka 40 iliyopita, kwa mujibu wa Shirika la Afya Duniani (WHO).

Ugonjwa wa kisukari hutokea wakati mwili hauwezi kutumia sukari inayotengenezwa na mwili (glucose) yote katika damu.

Kwa kawaida glucose yenyewe si mbaya, kwani nimafuta ya seli zote katika mwili kwa baadhi ya tishu, kutumia glucose hiyo, zinahitaji hatua ya insulini, ambazo ni homoni zinazozalishwa na kongosho ambayo inaruhusu sukari hiyo kupenya kwa urahisi zaidi ndani ya seli na hivyo kubadilishwa kuwa nishati.

Matatizo ya kisukari yanaweza kusababisha mshtuko wa moyo, kiharusi, upofu, kushindwa kufanya kazi kwa figo na kukatwa kwa viungo vya mwili.

Licha ya hatari, watu wengi wenye ugonjwa wa kisukari hawajui kuwa wanao. Mabadiliko ya mtindo wa maisha yanaweza kuzuia mtu kuugua kisukari.



# TAHARIRI

## Kwa hili CCM inastahili pongezi

WANACHAMA wa Chama Mapinduzi (CCM), sambamba na wananchi wote Tanzania wametakiwa kuwa makini na viongozi wenye tabia ya uchonganishi kwa kile walichodai baadhi yao kuchochea chuki inayoweza kuwatenganisha.

Hiyo ni kauli makini iliyotolewa na katibu wa NEC Itikadi, Uenezi na Mafunzo wa CCM Taifa ndugu Amos Makalla wakati akizungumza na Wananchi na wanachama wa Chama cha Mapinduzi katika Viwanja vya Umoja ni nguvu kusini Pemba ikiwa ni muendelezo wa ziara yake ya Mikoa 6 Visiwani Zanzibar.

Makalla pia amesema kuwa Dkt Samia Suluhu Hassan na Dkt Hussein Mwinyi hawana ubaguzi wowote kwenye suala la kuwaletea maendeleo lakini wenzetu kila kukicha wanaweka fitina na hili kazi kwenu Wazinzabar kwa ujumla wakataeni Viongozi hao na wanasiasa hao kwa kuwanyima kura wakati Uchaguzi utakapofika na tuchague chama cha mapinduzi ambacho ndio kina wajibu wa kuyaleta.

Kauli hii haistahili kupita bila kupongezwa ndiyo maama sisi JAMVI LA HABARI tunaipongeza kwa vile imezingatia kuleta umoja mshikamano na maelewano baina ya Watanzania.

Tunasema hayo tukijua kwamba kipindi kijacho yani Mwezi Oktona nchi itaingia katika kinyang'anyiro cha Uchaguzi Mkuu wa Rais, wabunge na Madiwani hivyo wasioitakia mema nchi wanaweza kutumia nafasi hiyo kuingiza chuki na hasama baina ya wananchi.

Tunaamini kila aliyesikia rai hii iliyotolewa na chama tawala, atazingatia kwa vile nchi hii ina wanasiasa na wasio wanasiasa ambao wanahitaji amani na utulivu.


## BODI YA UHARIRI

Mhariri Mkuu - 0762 178 678
Idara Ya Matangazo/Masoko - 0743 777 778,
- 0659 555 744
Idara Ya Usambazaji - 0676807684,
- 0787 288 160

Gazeti hili hutolewa na **JAMVI MEDIA GROUP**
S. L. P 78862, Dar es Salaam
**Tel:** +255 676 807684, 255 743 777778
**Email:** jamvinews@gmail.com
www.jamvilahabari.co.tz





*Waziri wa Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum, Dk. Dorothy Gwajima (katikati) akiwa katika mkutano na waandishi wa Habari kuelezea Maadhimisho ya Siku ya Wanawake Duniani kwa mwaka 2025.*

UCHAMBUZI

# Ushindi wa CCM unatokana na utekelezaji wa ilani yake

NA MWANDISHI WETU

SIRI kubwa ya maandalizi ya CCM Kushinda uchaguzi Mkuu na kuendelea kushika Doila, ni utekelezaji wa Ilani ya chama hicho ambayo viongozi, waliopewa nafasi waliibeba na kuifanyia kazi kila eneo.

Hilo ndilo linaloweza kuwafanya wagombea wa chama hicho akiwemo mgombea nafasi ya Urais Dkt Samia Suluhu Hassan pamoja na jopo la wviongozi wengine watakaopambania nafasi za Ubunge na Madiwani.

Tayari chama hicho kimefanya chaguzi za ndani kama vile ule uliohusisha Mkutano Mkuu wa CCM, ulimchagua Mzee Steven wassira kuwa Makamu Mwenyekiti wa chama hicho Bara.

Wassura aliyekuwa nje ya madaraka ya kisiasa kwa muda mrefu kwa maneno yake mwenyewe alieleza kushangazwa na ushindi ule na akaahidi kuifanya kazi hiyo kwa uadilifu na unyenyekevu mkubwa, kama hatua ya kulipa fadhjila na heshima ile kubwa.

Pia mkongwe huyo akatabiri ushindi wa kishindo utakaokipata chama chake, mtaji mkubwa ukiwa ni utekelezaji wa Ilani na jinsi chama hicho kinavyoendesha siasa zake kwa njia ya uwazi na uwajibikaji.

Mkongwe huyo ameingia na Falsafa ya Umoja Maridhiano na Ushindi, kazi ambayo amewaahidi wajumbe waliomuamini kushika wadhifa huo kuwa ataifanya kwa bidii kubwa huku akiamini ni jukumu lenye baraka za Mungu.

Kwa tathmini nyepesi ya ushindi huu wa Wasira una maana kubwa kwa CCM kuekelea uchaguzi Mkuu wa Rais, Wabunge na Madiwani utakaofanyika mwaka huu, mwezi Okttoba kwamba mtaji wake unaonekana umeongezeka

Ukichukulia kuwa CCM ndicho chama kinachoongoza nchini kwa kuwa na wanachama na wapenzi wengi kinaweza kutumia mtaji huo kumpa ushindi wa kishindo mgombea wake wa Urais na hata Wabunge na Madiwani.

CCM ina watu wengi hata isipohitaji kura ya wapinzani au watu wasiofungamana na siasa ya chama chochote bado wana uhakika wa kushinda hususa nafasi ya Urais pengine baadhi ya wabunge wachache wanaweza kupoteza viti kutokana na kutowafanyia vizuri wapiga kura wao katika kipindi kilichopita.

Mgombea wa CCM anasaidiwa na maendeleo yanayoonekana kila kona, atahitaji timu ya kawaida tu kumnadi na kuweza kumpa ushindi wa kimbunga kama huu alioanza kuonyesha dalili Mzee Wasira

Ushindi wa CCM mwaka huu unaonekana bila kuhitaji utafiti mkubwa, kwani hata ukiangalia upande wa upinzani bado unaonekana kama hakuna chama chenye nguvu kama ilivyokuwa katika chaguzi za awamu zilizoipita tangu kuanzishwa mfumo wa vyama vingi vya Siasa mwaka 1992

Licha ya CCM kujiandaa kama ilivyokuwa wakati wote inapoingia katika uchaguzi, lakini mwaka huu licha ya uwepo wa maridhiano ya kisiasa, lakini upinzani unaonekana kupoteza nguvu kuliko miaka yote ya uchaguzi.

Ni mwaka tutakaoendelea kusikia vishindo vya CCM katika majimbo na makelele ya wapinzani watakaoendeleza msamiati wa kuibiwa kura ili hali hawakuwa na maandalizi zaidi ya malumbano na kukashifiana.

# Sekta isiyo rasmi inavyoch



NA MWANDISHI WETU

TAKWIMU za Shirika la Kazi Duniani (ILO) za mwaka 2022, zineonyesha kuwa sekta isiyo rasmi nchini Tanzania imekuwa nguzo kuu ya uchumi wa taifa.

Sekta hii inachangia zaidi ya asilimia 50 ya Pato la Taifa huku pia ikitoa ajira kwa zaidi ya asilimia 80 ya wafanyakazi wake.

Mbobezi wa masuala ya fedha kutoka Ruislip, London Magharibi nchini Uingereza, Brianna Johnson anasema, "Sekta hii ina uwazi, ustahimilivu na uwezo wa asili wa kuondoa au kupunguza umaskini. Hata hivyo, bado kampuni nyingi zisizo rasmi ziko nje ya mfumo rasmi wa kodi."

Anasema hali hii ya kampuni nyingi kuwa nje ya mfumo wa kodi si lazima kwamba inatokana na ukwepaji kodi wa makusudi, bali inatokana zaidi na uwepo wa taratibu ngumu zenye urasimu, vikwazo vya kifedha na hofu kubwa ya kutozwa faini ya kikodi.

Makala haya leo yanashughulikia changamoto hizi kwa kuwasilisha mkakati wa kina wa maboresho ya kodi unaotokana na uchanganuzi wa kitaalamu na vipimo thabiti.

Lengo kuu la makala haya ni kuipa Tume ya Rais ya Maboresho ya Kodi maoni muhimu kutokana na mitazamo ya umma kuhusu ujumuishaji wa sekta isiyo rasmi ya nchini katika uchumi rasmi, na hatimaye kukuza zaidi mfumo jumuishi na endelevu wa kifedha.

Mazingira ya Kodi

Mtaalamu wa masuala ya kodi kutoka Algeria ambaye kwa sasa yuko likizo Karatu mkoani Arusha, Yasmine Yassine anasema mfumo wa kodi wa Tanzania hautabiriki na umepitwa na wakati mambo yanayofanya usifae kwa sekta isiyo rasmi. Anasema wakati Sheria ya Fedha ya 2020 ililenga kurahisisha usajili wa kodi, athari zake zimekuwa ndogo kwani wafanyabiashara wengi wameachwa nje ya mfumo rasmi.

Tathmini hiyo inaungwa mkono na mshauri wa masuala ya fedha aliyeko Babati mkoani Manyara, Hussein Kilokoza anayenukuu ripoti za KPMG na PwC za 2020 zinazobainisha kuwa, licha ya kuwapo maboresho ya kodi hivi karibuni, biashara nyingi hazijasajiliwa.

Kwa mujibu wa matokeo ya utafiti, Sheria ya Fedha haijaondoa vikwazo vya kimuundo vinavyokwamisha urasimishaji wa biashara zisizo rasmi. Matokeo hayo yanathibitisha zaidi hoja ya Yassine kuwa, mfumo wa ulipaji kodi uliopo Tanzania hauendani na hali halisi inayowakabili wafanyabiashara wadogo wanaofanya shughuli zao nje ya uchumi rasmi. Kwa msingi huo, uchanganuzi wa takwimu zilizopo unaonesha kuwa, asilimia kati ya 20 hadi 30 pekee ya biashara zisizo rasmi ndizo zimesajiliwa.

Utafiti kuhusu biashara isiyo rasmi uliofanywa na Benki ya Dunia mwaka 2023 ulibainisha biashara zisizo rasmi 2,433 katika maeneo kadhaa ya Dar es Salaam kwa kubaini ukubwa wa sekta hiyo. Kwa kuzingatiwa kuwa kwa

ujumla maeneo ya mijini yana viwango vya juu vya usajili kuliko vijijini, asilimia ya kitaifa inaweza kuwa chini. Hii inaonesha kuwa, biashara milioni 3.5 hadi 4 zisizo rasmi hazijasajiliwa na hivyo kuwapo hitaji la maboresho ya kodi yanayorahisisha usajili, ufikiaji wa fedha na maboresho yanayolenga kujenga imani. Urasimishaji unaweza kupanua wigo wa vyanzo vya kodi na kuzipa biashara usaidizi wa kifedha na motisha za serikali.

Mshauri wa masuala ya kodi anayeishi Dodoma, Brian Macha anasema watendaji wasio rasmi, wakiwemo wachuuzi wa mitaani (wamachinga) na madereva wa bodaboda huhama mara kwa mara na hivyo kuwa vigumu kwa mamlaka za kodi kufuatilia mapato na kutekeleza wa kanuni na sheria za kodi.

Kimsingi, mtindo au mfumo wa kodi uliopo umeshindwa kumudu mabadiliko ya mara kwa mara ya mtiririko wa

fedha katika sekta rasmi, hivyo kuzitenganisha zaidi biashara zisizo rasmi. Ni muhimu kuwapo mtazamo unaobadilika ili kukuza ushirikiano endelevu wa kiuchumi.

Vikwazo utekelezaji sheria za kodi

Kwa mujibu wa Brian Macha, kutegemea mzunguko wa fedha wa kila siku na ukosefu wa huduma za kifedha hufanya ulipaji kodi ku
changamoto kwa wamiliki wa bias
ra zisizo rasmi. Hii ni kwa kuwa w
fanyabiashara wengi huogopa w
idhani kuwa, urasimishaji biash
utawapa mizigo wa kodi isiotabir
na kuathiri faida kidogo wapatayo

Aidha, kutoaminiwa kwa mam
ka za kodi kutokana unyanyasaji,
toza kodi bila utaratibu na usimam
usioeleweka hupunguza utekelez
wa sheria za kodi. Taarifa zinaones
kuna asilimia 25 ya wafanyabiash
wasio rasmi wa mijini katika nchi 5
juu kiuchumi barani Afrika.

Nchi hizo ndizo zinazojenga a

# hochea ukuaji wa uchumi



"Kupitia mfumo ambao ni rafiki kwa watumiaji, Tanzania inaweza kufikia ongezeko la asilimia 40-50 la usajili wa biashara ndani ya miaka mitano hadi saba ijayo, mradi tu kutakuwa na usimamizi thabiti wa sera na msaada."

imia 50 ya Pato la Taifa la Afrika la Dola za Marekani trilioni 2.4 wanakumbwa na unyanyasaji unaohusiana na masuala ya kodi, hivyo kuweka vikwazo katika usajili. Brian anasema bila kuwapo elimu sahihi na endelevu kuhusu masuala fedha, ufikiaji bora wa huduma za kibenki na muundo wa kodi ulio wazi, itakuwa vigumu kwa biashara nyingi kurasimishwa.

Mfumo saidizi na unaotabirika ni muhimu ili kuchochea utekelezaji wa masuala ya kodi. Musa ambaye ni mwanauchumi anayeishi Nyanda za Juu Kusini, anasema hofu ya kodi ya juu kupita kiasi ni kikwazo kingine kikubwa kwa wajasiriamali wasio rasmi wanaohofia urasimishaji kuwawekea mizigo mingi ya kodi na adhabu kali mambo yanayoweza kuathiri zaidi faida ndogo waipatayo.

Utafiti wa Taasisi ya Financial Sector Deepening Trust Tanzania unaonesha kuwa, wajasiriamali hao wengi hususani wanawake hukabiliwa na unyanyasaji ukiwamo wa matusi na shinikizo kutoka mamlaka za mitaa.

Aidha, madai ya rushwa pia hukatisha tamaa na kuwavunja moyo wajasiriamali dhidi ya utekelezaji wa sheria za kodi. Utafiti uliofanywa na Ilona Steiler mwaka 2018 na kuchapishwa katika jarida la 'Articulo – Journal of Urban Research,'unabainisha hatari zinazowakabili wafanyabiashara wa mitaani Dar es Salaam kutokana na kuonekana kwao kwa wingi.

Utafiti huo uitwao 'Kuna nini katika Neno? Dhana ya Siasa ya Biashara Isiyo Rasmi Dar es Salaam,' unabainisha kuwa, mara kwa mara wafanyabiashara hutozwa faini kali, hufanyiwa unyanyasaji wa kimwili na hata kufunguliwa mashitaka ya jinai na kuadhibiwa hadi miezi sita jela.

Wakati mwonekano wa wajasiriamali hao ukisaidia kuvutia wateja, pia huwaweka katika hatari ya kuchukuliwa hatua za kisheria. Changamoto hizi huchochea kukosekana imani kwa mamlaka za kodi na kuondoa ari ya ulipaji kodi kwa hiari, hivyo kuongeza pengo kati ya uchumi usio rasmi na uchumi rasmi.

Ili kuondoa vikwazo hivi vya kimfumo, hapana budi yafanyike maboresho ya kodi yenye ufanisi.

Kurahisisha mchakato wa usajili

Jambo la msingi katika maboresho ya msingi ya kodi ili kuimarisha utekelezaji wa kanuni na sheria za kodi ni kurahisisha mchakato wa usajili wa biashara ambao bado ni kikwazo kikubwa kwa wajasiriamali.

John Marwa ambaye ni mtafiti aliyeko Geita, anasema nafasi ya Tanzania ya 141 kati ya uchumi 190 katika ripoti ya Benki ya Dunia ya 'Doing Business 2020' inaonesha vikwazo vikubwa vya ukiritimba vinavyozuia urasimishaji wa biashara.

Nafasi hiyo inaonesha ugumu wa taratibu za udhibiti zinazokatisha tamaa wamiliki wa biashara nyingi zisizo rasmi

kuingia katika uchumi rasmi. Hata hivyo, mwaka 2021 Benki ya Dunia ilisitisha Fahirisi ya Urahisi wa Kufanya Biashara.

Kwa mujibu wa Marwa, nafasi ya awali ya Tanzania inadhihirisha hitaji muhimu la kuboresha na kurahisisha michakato wa usajili na kufanya iwe inayopatikana kirahisi na kwa uwazi kusimamia utekelezaji wa sheria za kodi.

Naye mwanauchumi mstaafu anayeishi katika Kaunti ya Kilifi nchini Kenya, Caleb Abraham anapendekeza mfumo wa usajili uliorahisishwa ujumuishe mfumo wa kodi wa ngazi moja kadiri ya viwango vya mapato ili kuziwezesha biashara zisizo rasmi kufika katika uchumi rasmi.

Anasema kuunganisha mifumo ya usajili na malipo kwa njia ya simu kutapunguza vikwazo vikiwamo vya urasimu, utapunguza ubebaji na matumizi ya karatasi (mafaili) na kusaidia kukabili rushwa sambamba na kujenga mfumo wa kodi wenye uwazi na ufanisi zaidi. Uanzishaji wa vituo maalumu vya usajili wa kodi katika ngazi ya serikali za mitaa utasaidia kutoa msaada wa moja kwa moja kwa wafanyabiashara binafsi, utarahisisha mchakato na utabainisha manufaa ya muda mrefu ya urasimishaji.



Profesa mmoja wa Shule ya Uchumi ya Chuo Kikuu cha Makerere (MakSOE) nchini Uganda, anasema kurahisisha usajili wa kodi ni zaidi ya uimarishaji wa kiutawala na ni zana yenye nguvu ya uwezeshaji wa kiuchumi.

Anafafanua, "Kupitia mfumo ambao ni rafiki kwa watumiaji, Tanzania inaweza kufikia ongezeko la asilimia 40-50 la usajili wa biashara ndani ya miaka mitano hadi saba ijayo, mradi tu kutakuwa na usimamizi thabiti wa sera na msaada."

Kwa mujibu wa msomi huyo, katika biashara milioni 1.3 iliyosajiliwa sasa, ongezeko la asilimia 50 litaongeza idadi hiyo na kufikia takriban milioni 1.95 hivyo kupanua vyanzo kodi na mapato ya taifa.

Ulipaji kodi kwa awamu

Wachambuzi nchini wanasema mtindo wa ulipaji kodi kwa awamu ni njia ya kisayansi na isiyotisha biashara zisizo rasmi kuingia katika sekta rasmi. Ramadhani Kaniki wa Manyara anasema badala ya kuweka mzigo wote wa kodi

mara moja kwenye biashara, uanzishwe taratibu wa kulipa taratibu madeni ya kodi ili kuzipa kampuni ndogo uwezo wa kumarika kifedha na kukua.

Joyce Mangi wa Arusha Arusha anaunga mkono hoja hiyo akipendekeza mfano wa viwango vya kodi. Anasema biashara ndogo zinazopata chini ya Sh milioni 7 kila mwaka zipewe msamaha wa kodi wa miaka mitatu ili biashara hizo zipate muda na nafasi ya kujiimarisha kabla ya kuanza majukumu ya kodi.

Wakati huo huo, biashara zinazozalisha zaidi ya Sh milioni 7 na si zisizoidi Sh milioni 20 wafaidike kutokana na kupunguza viwango vya kodi katika kipindi cha mpito, hivyo kuwapunguzia mzigo wa kifedha na kuhimiza urasimishaji.

Mchambuzi wa kikanda wa masuala ya uchumi wa Rwanda anasisitiza kuwa, ulipaji kodi kwa awamu utasaidia biashara kuwa na utulivu wa kifedha na kuchochea urasimishaji. Anasema ingawa hakuna takwimu maalumu kuthibitisha athari za moja kwa moja, nchini Rwanda maboresho ya kodi yamechochea utekelezaji wa sheria za kodi.

Kwa mujibu wa Ripoti ya Shirika la Kimataifa la Fedha (IMF) ya Mwaka 2023, uwiano wa kodi kwa Pato la Taifa pia umeongezeka maradufu kutoka chini ya asilimia 8 katika miaka ya 1990 hadi zaidi ya asilimia 16 mwaka 2020.

Ripoti ya Wizara ya Fedha na Mipango ya Kiuchumi ya 2023 inasema kujumuisha usajili wa kodi na utoaji leseni za biashara kumepunguza vikwazo vya ukiritimba. Kwa Tanzania, mfumo wa kodi wa awamu utaongeza kasi ya usajili wa biashara kwa asilimia 20-28 katika kipindi cha miaka miwili kutoka usajili wa sasa wa milioni 1.3 hadi katika ya milioni 1.56 na milioni 1.66.

Ukuaji huu unaweza kuongeza mapato ya kodi kwa asilimia 15-20, ikizingatiwa kuwa biashara mpya huchangia kwa uwiano sawa. Ingawa mafanikio hutegemea utekelezaji na mwitikio wa biashara, maboresho ya Rwanda yanaonesho umuhimu wa kurahisisha taratibu za kodi na usajili ili kuchochea urasimishaji na ukuaji wa mapato nchini.

Hitimisho

Kimsingi, sekta isiyo rasmi ya Tanzania ni nguzo muhimu ya shughuli za kiuchumi, ambayo ujumuishwaji wake katika mfumo wa kitaifa wa fedha unahitaji mbinu za kimkakati, ulipaji kodi wa awamu na maboresho ya kodi. Kutokana na maoni hayo ya kitaalamu na data, maboresho hayo yanaweza kuongeza utekelezaji wa sheria za kodi, kuongeza mapato ya serikali na kujenga mazingira yanayowezesha biashara ndogo kustawi kwa njia endelevu.

Mbinu ya muundo bora si tu kwamba itaziba pengo kati ya wajasiriamali wasio rasmi na uchumi rasmi, bali itaongeza utulivu wa uchumi muda mrefu.

# WANAFUNZI SUA WANUFAIKA NA UFADHILI




FARIDA MANGUBE, MOROGORO

MAKAMU Mkuu wa Chuo Kikuu cha Sokoine cha Kilimo (SUA), Prof. Raphael Chibunda, amewataka wanafunzi waliopata ufadhili wa masomo kutoka taasisi ya CAN TANZANIA kutumia fursa hiyo kwa bidii, kuwa na nidhamu, na kuhakikisha wanafikia malengo yao ya kielimu.

Prof. Chibunda alitoa wito huo wakati wa uzinduzi wa kampeni ya ufadhili wa masomo kwa wanafunzi wanaosaidiwa na CAN TANZANIA. Amesisitiza kuwa SUA ni miongoni mwa taasisi za elimu zilizonufaika na mpango huo, huku akihimiza taasisi hiyo kupanua wigo wa ufadhili ili kuwafikia wanafunzi wengi zaidi wanaokabiliwa na changamoto za kifedha.

Mwenyekiti wa Bodi ya CAN Tanzania, Dkt. Catherine Aloyce Masau, amesema kuwa shirika hilo limefadhili wanafunzi 36 kutoka vyuo mbalimbali nchini, vikiwemo vya Tanzania Bara na Zanzibar. Ufadhili huo unahusisha wanafunzi wa ngazi tofauti za elimu, ikiwemo shahada za uzamili, diploma, na vyeti. Amebainisha kuwa mpango huo unawalenga wanafunzi wa jinsia zote, hasa wale kutoka familia zenye hali duni.

"Watanzania wengi wanakabiliwa na changamoto za kugharamia masomo yao na mara nyingi hutegemea ufadhili wa serikali. Kama CAN Tanzania, tumeona ni muhimu kusaidia juhudi hizo kupitia mpango huu wa ufadhili," alisema Dkt. Masau.

Kwa upande wake, Mkurugenzi Mkuu wa CAN Tanzania, Dkt. Sixbert Mwanga, alieleza kuwa vigezo muhimu vya kupata ufadhili ni hali ya kifamilia ya mwanafunzi na kozi anayosomea, ambayo inapaswa kuwa na mchango wa moja kwa moja katika jamii.

Aliongeza kuwa wanafunzi wanaofadhiliwa wanapaswa kudumisha viwango bora vya ufaulu ili kuendelea kunufaika na mpango huo.

Mmoja wa wanufaika wa ufadhili huo, Ampelius Anthony, mwanafunzi wa Tiba ya Mifugo SUA, alieleza kuwa safari yake ya elimu ilikuwa na changamoto kubwa, lakini kupitia ufadhili huo, sasa anaweza kuendelea na masomo yake bila vikwazo vya kifedha.

"Ufadhili huu umekuja wakati sahihi na utanisaidia kutimiza malengo yangu ya kielimu," alisema Ampelius.

Aidha, alitoa wito kwa mashirika mengine kuiga mfano wa CAN Tanzania kwa kusaidia wanafunzi wenye uhitaji ili kuwasaidia kufanikisha ndoto zao.

Mpango huu wa ufadhili kutoka CAN Tanzania umeleta faraja kwa wanafunzi wengi nchini, huku ukihamasisha bidii katika masomo na kuwasaidia vijana wa Kitanzania kujenga mustakabali mzuri wa maisha yao.

> "Ufadhili huu umekuja wakati sahihi na utanisaidia kutimiza malengo yangu ya kielimu," alisema Ampelius.



# SERIKALI YASISITIZA MFUMO WA KISASA KUSIMAMIA MAZAO

NA ALEX SONNA-DODOMA

WAZIRI wa Viwanda na Biashara, Mhe. Dkt. Selemani Jafo ameitaka Bodi ya Usimamizi na Stakabadhi za Ghala kuusimamia Mfumo wa kutumia kamera za kidijitali na stika ya utambuzi wa ghala ili wanunuzi waweze kuuamini huku akiwataka watumishi wa Taasisi hiyo kuacha alama katika utendaji kazi wao.

Dkt.Jafo ametoa kauli hiyo leo Januari 31,2025,Jijini Dodoma wakati akizungumza katika Uzinduzi wa Mfumo wa kutumia kamera za kidijitali na stika ya utambuzi wa ghala.

Waziri Jafo ametaka Mfumo huo uwe imara ili kuongeza uaminifu kwa wateja na kuweza kuona Kila kitu kilichopo katika ghala lako.

"Mkurugenzi (Asangye Bangu) huu mfumo uwe imara tutengeneze kujiamini kwa wanunuzi na tuwatafute vijana wa tehama, Mteja atachokiona ndio kiwe uhalisia hatutaki ukanjanja…mmefanya jambo kubwa.Mtaendelea kufanya ubunifu imani kubwa mtafanya connection nzuri.Mimi sina mashaka na jinsi mnavyoenda,"amesema Waziri Jafo

Hata hivyo, Dkt. Jafo ameipongeza Taasisi hiyo kwa kufanya vizuri pamoja na kukutana na changamoto mbalimbali kwani inaashiria utendaji kazi mzuri.

"Wakulima walikuwa wanasema Mbaazi hainunuliki lakini kupitia Mfumo wa Stakabadhi ghalani umefanya vizuri, Mkurugenzi Mtendaji Bangu nakupa maua yako mmefanya vizuri.

Amesema kipindi cha nyuma korosho zilichanganywa na mawe kupelekea kutaka kuharibu soko la zao hilo nje lakini Sasa hivi mambo yanaenda vizuri.

Amesema kupitia Mfumo huo mnunuzi anaweza kuona hata akiwa nje ya Tanzania.

Dkt.Jafo amewaomba wale wanaosimamia maghala kuweka logo ili Mfumo huo uweze kufanya vizuri zaidi.

Kuhusu watendaji wa Serikali, Dkt.Jafo amewataka kuendelea kufanya vizuri zaidi huku akaigiza Kila mtumishi kufanya kazi kwa bidii ili kuacha alama.




"Niwaambie muda tunautumia katika kazi leo kuna mtumishi anaomba likizo siku 28 weka mashaka kama atakukubalia, tengenezeni Utamaduni kazi zinaenda vizuri.Imani ya gu Kila mmoja atatimiza wajibu wake.

"Fanya kazi acha legacy hakikisha mtu anaekuja kiatu kisimtoshe.Fanya kazi kama ni ibada.Fanyeni kazi tulete mabadiliko,"amesema Waziri Jafo.

Kwa upande wake Mkurugenzi Mtendaji wa Bodi ya Usimamizi wa Stakabadhi za Ghala, Bw.Asangye Bangu, amesema kazi yao kubwa ni kuwezesha biashara pamoja na kutoa leseni huku akidai sababu ya uwepo wao ni kurasimisha masoko, kuwezesha wakulima kulipwa vizuri, kuongeza ubora na hivyo kuongezeka kipato kwa watanzania.

Amesema mwaka huu wameshuhudia ongezeko la mapato katika mazao yanayotumia Mfumo.

Amesema wamejipanga na Wizara ya mifugo kuingiza zao la Mwani na samaki pamoja na Madini katika Mfumo huo.

"Nikuhakikishie tumesimama imara na tunaendelea kutekeleza kwa ufasaha.Maelekezo yako tutayafanyia kazi na kuyapokea,"amesema Bw. Bangu

Naye Meneja Uratibu na Huduma kutoka Bodi ya Usimamizi wa Stakabadhi za Ghala Bw.Abubakari Ndwata, amesema stika ya utambuzi kazi yake ni kutoa taarifa, jina la ghala, umiliki, mahali lilipo, mtu anaweza kuingia ndani ya ghala ili aweze kuona, zao kwa wakati huo, kiasi cha mzigo, idadi ya magunia na uzito wa magunia.

"Nembo hii ya utambuzi inaenda kuongeza uaminifu wetu ili wanunuzi wawe wanajiamini, Mheshimiwa Waziri Jafo umeona tumeuza korosho nyingi,"amesema Bw.Ndwata

WAZIRI wa Viwanda na Biashara, Mhe.Dkt. Selemani Jafo, akizungumza wakati akizindua Mfumo wa kutumia kamera za kidijitali na stika ya utambuzi wa ghala, hafla iliyofanyika leo Januari 31,2025 jijini Dodoma.

# KAMPENI YA UIBUAJI WA WAGONJWA WA KIFUA KIKUU

NA MUHIDIN AMRI, TUNDURU

WIZARA ya Afya kupitia mpango wa Taifa wa kudhibiti Kifua Ki kuu na Ukoma imesema, kampeni ya mpango harakishi wa uibuaji Wagonjwa wa Kifua Kiku u itawafikia watu wote walioba inika kuwa na maambukizi ya ugonjwa huo ambao hawakufikiwa mwaka 2024.

Watu hao, wataanzishiwa Dawa ha raka kwa ajili ya kuzuia uweze kano wa kuambukiza watu wengin e ili kuifanya Tanzania kuwa nchi salama bila kuwa na watu walioambukizwa ugonjwa wa kifua kikuu ifikapo mwaka 2 030.

Hayo yamesemwa jana na Mwakili shi wa Wizara ya Afya kitengo cha kudhibiti Kifua Kikuu na Ukoma Dkt Jacob Mwanamtwa, baada ya kukagua utekelezaji wa kampeni hiyo katika maeneo mbalimbali ya wilaya ya Tunduru Mkoani Ruvuma.

Alisema, Wizara ya Afya imejipa nga na itahakikisha inawapata wagonjwa ambao hawakupatikana mwaka 2024 na kuwaanzishia matibabu yanayotolewa bure kwenye vituo vya Afya na Hospitali zote hapa nchini.

"Wagonjwa ambao hawajapatiwa m atibabu wanaendelea kuambukiza watu wengine katika jamii yetu na mbaya zaidi mgonjwa ambaye hajaanza kutumia Dawa anaweza kuambukiza watu kati ya 10 hadi 15 kwa mwaka" alisema Dkt Jacob.

Alisema, wameanza kampeni hiyo kwenye mikoa tisa hapa nchini ambayo haikufanya vizuri katika kuibua wagonjwa wa kifua kikuu mwaka jana ikiwemo Mkoa wa Ruvuma na kupitia kampeni hiyo wagonjwa wote watafikiwa ili waweze kuanzish iwa matibabu.

Alisema, malengo ya Shirika la Afya Duniani(WHO) kutokomeza ugonjwa huo ifikapo mwaka 2030 , lakini kutokana na changamoto mbalimbali yanaweza yasifikiwe au yakafanikiwa kutokana na mikakati iliyowekwa na Serikali yetu kupitia Wizara ya Afya.

Mratibu wa Kifua Kikuu na Ukom a wa Wilaya ya Tunduru Dkt Mkasange Kihongole alisema, kupitia kampeni ya mpango harakishi watahakikisha wananchi wote wanapata elimu ya kifua kikuu, wanafanyiwa uchunguzi na ambao watabainika kuwa na vimelea vya ugonjwa huo wataanzishiwa dawa.

*Muhudumu wa afya ngazi ya jami i Idd Yakiti(Nyuki) alisema, kwenye kampeni ya uibuaji wa Wagonjwa wa Kifua Kikuu kazi anayofanya ni kwenda kwenye zahanati ili kuchukua makohozi ya wahisiwa na kuzifikisha Hospitali ya wilay a kwa ajili ya uchunguzi.*



"katika kipindi hiki cha mpito ambacho tunatakiwa kufanya kazi kwa juhudi kubwa tumeanza kuangalia maeneo hatarishi zaidi, baada ya hapo wataalam tutasambaa kwenye maeneo mengine ambayo siyo hatarishi lakini kuna watu ambao wako kwenye hatari ya kupata ugonjwa huo"alisema Mkasange.

Mkasange ametaja maeneo hatari shi ni kwenye maboma ya wafuga ji, vijiwe vya boda boda, wachez a bao, Pooltable machimbo ya madini na maeneo mengine yenye mikusanyiko ya watu kuanzia watano na kuendelea.

Aidha alisema, kabla ya Wizara ya Afya kuzindua mpango haraki shi wa kuibua wagonjwa wa TB, Wilaya ya Tunduru imeshaanza kutekeleza kampeni hiyo kwenye vijiji vyote vinavyozun gukwa na machimbo ya madini, shule za Msingi na Sekondari za bweni.

Mkasange alisema, walianza kamp eni ya uelimishaji, uibuaji na uchunguzi wa TB mapema ili kwenda na kasi ya mpango harakishi wa uibuaji Wagonjwa wa Kifua Kikuu iliyozinduliwa wiki iliyopita ili kukata mnyororo wa maambukizi katika wilaya ya Tunduru.

Naye Mratibu wa huduma za maab ara Mkoa wa Ruvuma Said Kaunde alisema, kampeni ya mpango harakishi ya uibuaji Wagonjwa wa Kifua Kikuu imegawanyika kwenye makundi mawili ambayo ni kuwafikia Wananchi wenye vimelea vya TB kwa ajili ya kuchukua sampuli za makohozi na kuwaanzishia Dawa.

Alisema, katika mkakati wa kuto komeza ugonjwa huo Serikali yetu imewekeza fedha nyingi kwenye vifaa tiba hasa kununua mashine za kisasa za uchunguz i wa vimelea vya kifua kikuu na katika Mkoa wa Ruvuma kuna mashine 11 ambazo zimepelekwa kwenye Halmashauri zote nane.

Pia alisema, tangu kampeni hiyo ilipoanza hadi sasa wamefanik iwa kukusanya sampuli zaidi ya 851 ambazo baada ya kupelekwa maabara kwa ajili ya uchunguzi,24 zimekutwa na maambukizi ya ugonjwa huo.

Muhudumu wa afya ngazi ya jami i Idd Yakiti(Nyuki) alisema, kwenye kampeni ya uibuaji wa Wagonjwa wa Kifua Kikuu kazi anayofanya ni kwenda kwenye zahanati ili kuchukua makohozi ya wahisiwa na kuzifikisha Hospitali ya wilay a kwa ajili ya uchunguzi.

Nyuki, ameipongeza Serikali kup itia Wizara ya Afya kwa kuchuk ua hatua katika kukabiliana na ugonjwa huo ambao ni miongoni mwa magonjwa kumi Ulimwenguni yanayoongoza kusababisha vifo vya watu wengi.



# MIKOANI NI DKT SAMIA, DKT MWINYI NA CCM 2025



NA MWANDISHI WETU

CHAMA Cha Mapinduzi (CCM) Mkoani hapa kimeunga mkono uamuzi wa Mkutano Mkuu wa CCM Taifa kuwapitisha Dkt Samia Suluhu Hassan, Dkt Hussein Mwinyi na Dkt Nchimbi kuwa wagombea Urais kupitia CCM mwaka huu.

Pongezi hizo zimetolewa na Viongozi mbalimbali wa chama hicho kwenye maandamano ya amani yaliyofanyika juzi mjini hapa ambapo walieleza kuwa hatua hiyo imetokana na kasi na weledi mkubwa walioonesha katika utendaji wao.

Mwenyekiti wa CCM Mkoa wa Tabora Said Mkumba amesema kuwa wamefanya maandamano hayo ili kuunga mkono uamuzi huo kwa kuwa viongozi hao 2 wameonesha uwezo mkubwa na kusimamia kwa asilimia 100utekelezaji ilani.

ëUamuzi huo ni ishara tosha kwamba wanaCCM tumeridhishwa na uwezo wao na kasi yao ya kusimamia utekelezaji ilani ya uchaguzi ya CCM ya mwaka 2020-2025 kwa asilimia 100 na tuna imani kubwa kwaoí, ameeleza.

Amebainisha kuwa uamuzi huo unamaanisha kwamba Rais Samia na Mgombea mwenza Dkt Nchimbi ndio chaguo la wanaCCM kwenye urais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Rais Mwinyi kwenye urais wa Zanzibar.

Nkumba ameeleza kuwa kasi ya maendeleo yaliyoletwa na Rais Samia na Rais Mwinyi kule Zanzibar ni kielelezo tosha kuwa Viongozi hawa wanatosha kupewa mitano tena na huo ndio uamuzi wa mwisho wa wanaCCM wote.

ëRais Samia ni mwanamke shujaa na kiongozi makini mwenye maono makubwa ya kimaendeleo, tumepokea uteuzi huo kwa mikono miwili, Tabora tunaunga mkono mapendekezo hayo kwa asilimia 100í, amesema.

Mjumbe wa Halmashauri Kuu ya CCM Mohamed Nassoro amesema kuwa CCM ni chama imara na kitaendelea kuchagua Viongozi makini, wazalendo, wachapa kazi, wanaojali watu na siyo maslahi binafsi na wenye kauli safi.

Amebainisha kuwa Rais Samia, Rais Mwinyi na Emanuel Nchimbi ni chaguo sahihi, wana kila sifa zinazotakiwa na watanzania wote na wameonesha uwezo mkubwa katika utendaji wao.

ëWatanzania wana kila sababu ya kuwashukuru wajumbe wa Mkutano Mkuu kwa maamuzi hayo ambayo yatawapa nafasi wagombea hao wa CCM kujipanga vizuri kwa ajili ya uchaguzi mkuu utakaohusisha vyama vya upinzanií, amesema.

Naye Katibu wa CCM Mkoa Wilson Nkambaku ameeleza kuwa wajumbe wa Mkutano Mkuu wameonesha ukomavu mkubwa wa kisiasa na huo ndio ukweli, hata katiba ya chama inawapa nafasi ya kuendelea kushika nafasi hiyo.

Amebainisha kuwa wapinzani hawajawa na uwezo wa kuongoza nchi, hivyo akawataka kuendelea kujifunza kwa Chama Cha Mapinduzi hadi watakapokuwa na uwezo wa kujisimamia huku akiongeza kuwa serikali ya CCM itaendelea kuwaletea maendeleo wananchi pasipo kujali itikadi zao.

Mbunge wa Jimbo la Shinyanga Mjini, Patrobas Katambi, amesoma taarifa ya utekelezaji wa Ilani ya Uchaguzi ya Chama Cha Mapinduzi (CCM) 2020/2024, akisema ameitekeleza kwa asilimia 100.

Taarifa hiyo aliwasilisha leo Januari 24, 2025, mbele ya Wajumbe wa Mkutano Mkuu wa CCM Jimbo la Shinyanga Mjini, ambapo Katibu Mkuu wa Jumuiya ya Wazazi CCM Taifa, Ally Hapi, alikuwa mgeni rasmi.

Katambi, ambaye pia ni Naibu Waziri wa Ofisi ya Waziri Mkuu (Kazi, Vijana, Ajira na Watu Wenye Ulemavu), amebainisha mafanikio katika sekta mbalimbali, ikiwemo elimu, afya, miundombinu, maji, na nishati safi ya kupikia.

Elimu

Mbunge Katambi amesema ndani ya miaka minne, shule mpya tisa zimejengwa, zikiwemo shule za msingi tano na sekondari nne. Aidha, alifanikiwa kuanzisha tawi la Chuo cha Serikali za Mitaa Hombolo na kupanua Chuo Kikuu cha Moshi (KICoB) tawi la Kizumbi.

Miundombinu

Katambi ameeleza kuwa miundombinu ya barabara, madaraja, na masoko imeboreshwa. Alitaja ujenzi wa Uwanja wa Ndege wa Ibadakuli, daraja la Uzogole, na maboresho ya barabara katika maeneo ya Iwelyangula, Ibinzamata, Ndala, Ihapa, Mwamalili, na Mwanoni.

Afya

Ameboresha huduma za afya kwa kujenga vituo vya afya, zahanati sita, na hospitali, ikiwemo Kituo cha Afya Kambarage na Hospitali ya Rufaa ya Mkoa wa Shinyanga. Pia, alitoa ambulensi sita kwa msaada wa Rais Samia Suluhu Hassan.

Maji

Amesema mtandao wa maji umeongezwa katika maeneo ya Bugwandege, Masekelo, Mwamasheke, Mwanubi, Busongo, na maeneo ya mjini. Zaidi ya shilingi bilioni 195 zimetengwa kwa usambazaji wa maji kwa kipindi cha 2024/2025.

Mikopo na Ajira

Ameeleza kuwa shilingi milioni 200 zilitolewa kwa vikundi vya Boda boda, Bajaji, wanawake, na watu wenye ulemavu kupitia Halmashauri ya Manispaa ya Shinyanga. Pia, milioni 19 zilipatikana kupitia Ofisi ya Waziri Mkuu.

Nishati Safi

Katambi amegawa mitungi ya gesi 1,780 kwa makundi mbalimbali ili kuhamasisha matumizi ya nishati safi ya kupikia.

Michezo

Mbunge huyo alianzisha ligi mbalimbali za michezo, ikiwemo utoaji wa zawadi za hadi shilingi milioni 6 kwa washindi wa mashindano.

Katambi amewataka wana-CCM kushirikiana kwa ajili ya maendeleo na kuepuka migogoro. Aliwasihi viongozi wa chama kuendelea kushirikiana kwa manufaa ya wananchi.

Katibu wa CCM Mkoa wa Shinyanga, Odilia Batimayo, amempongeza Katambi kwa kazi nzuri na alionya dhidi ya kampeni za mapema za kugombea ubunge. Ally Hapi naye alimsifu Katambi kwa utekelezaji mzuri wa Ilani ya CCM, akisema mafanikio hayo yanaongeza imani ya wananchi kwa chama.

Hapi amewataka wagombea kuzingatia maadili ya chama, kujiepusha na wapambe wa kisiasa, na kuendeleza siasa za kisayansi kwa kujenga hoja kwa wananchi.

Katika hafla hiyo, Katambi pia amekabidhi kiti mwendo kwa mtoto mwenye ulemavu, Delfina Mashaka, na vifaa vya sauti kwa uongozi wa Stendi ya Mabasi ya Mkoa wa Shinyanga.

# Michezo Kimataifa

## Tetesi za soka




MANCHESTER United wameomba kufahamishwa kuhusu mustakabali wa mshambuliaji wa Chelsea na Ufaransa Christopher Nkunku, 27, huku winga wa Argentina Alejandro Garnacho, 20, akihusishwa na uhamisho wa kwingineko.



JUVENTUS wameipa Chelsea ruksa ya kumsajili kiungo wa kati wa Brazil Douglas Luiz, 26, ambaye pia ananyatiwa na Manchester City na Arsenal, hii imetokana na mazungumzo mazuri kati ya klabu hizo na pia maslahi yaliyoridhiwa na pande hizi mbili.




1

MSHAMBULIAJI wa Uingereza Marcus Rashford, ambaye amejiunga na klabu ya Aston Villa kwa mkopo, huenda asicheze tena Man United kwa vile uhusiano kati ya mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 27 na timu hiyo ya Old Trafford umesambaratika. (Guardian)

BAADA ya kulaulimiwa kwa muda mrefu kuwa tatizo la Arsenal ni kudharau kufaya usajili hasa eneo la ufungaji, hatimaye klabu hiyo imesikia kilio hicho na sasa imeanza mawindo makali ili kutibu pengo lililopo, kufutia mkakati huyo klabu hiyo imeingia chimbo na kumnasa Straika makali Raia Slovenia anayekipiga katika klabu ya RB Leipzig ya Ujerumani






## JOSEPH KANIKI 'GOLOTA' MPACHIKA MABAO ALUYEACHA HISTORISA SIMBA

NA HENRY PAUL

UKIWAULIZA wanachama na mashabiki wa Simba, kuwa miaka ya 2000 mwanzoni ni mpachikaji mabao gani wa timu yao aliyekuwa na mashuti makali, ni dhairi watakuambia kuwa ni Joseph Kaniki au 'Golota' kama mashabiki hao wa Kariakoo, mtaa wa Msimbazi walivyozoea kumwita.

Mpachikaji mabao huyo aliyekuwa na mwili mkubwa wa kimichezo, alikuwa na kila kitu ambacho mshambuliaji mahiri anatakiwa kuwa navyo, ambavyo si uwezo mkubwa wa kupachika mabao pekee, bali pia mashuti makali na kutumia nguvu pale inapohitajika.

Mkongwe huyo pamoja na kuanza kujulikana kidogo akiwa na timu za mitaani huko Mburahati, lakini umaarufu mkubwa alianza kuupata alipojiunga na Simba mwaka 2000.

Wakati alipojiunga na Simba, miongoni mwa wachezaji aliowakuta na kucheza nao ni Mohamed Mwameja, Ivo Mapunda, George Masatu, Twaha Hamidu 'Noriega', Boniface Pawasa, Amri Said 'Stam', Shekhan Rashid, Athumani Machupa, Said Maulid 'SMG', Issa Manofu na wengine wengi.

Pamoja na 'Golota' kujiunga na Simba mwaka 2000, lakini umaarufu mkubwa katika klabu hiyo alianza kuupata mwaka uliofuata wa 2001, katika mchezo wa watani wa jadi, Simba dhidi ya Yanga.

Katika mchezo wa kwanza wa watani hao wa jadi Simba dhidi ya Yanga, uliochezwa katika Uwanja wa Taifa jijini Dar es Salaam (sasa Uhuru), Septemba 1, 2001, Simba iliibuka kwa ushindi wa bao 1-0 na bao hilo pekee lilifungwa na mshambuliaji huyo Kaniki katika dakika ya 76.

Achilia mbali mchezo huo wa kwanza dhidi ya Yanga, pia nyota huyo alionesha makeke yake katika mchezo wa marudiano, uliochezwa Septemba 30, 2001, katika Uwanja wa CCM Kirumba, mjini Mwanza.

# Michezo Kimataifa



# DAVIES MWAPE ALIPELEKA MAJONZI MSIMBAZI 2011

NA HENRY PAUL

MIONGONI mwa matukio yaliyowahi kuwafurahisha wanachama na wapenzi wa klabu ya Yanga, moja ni lile la timu yao yenye maskani yake makuu Kariakoo, makutano ya mitaa ya Jangwani na Twiga, kumfunga mtani wake wa jadi Simba bao 1-0.

Mchezo huo ambao ulikuwa ni mkali na wa kusisimua kwa muda wote wa dakika 90, ulichezwa siku ya Jumamosi Oktoba 29, 2011, katika Uwanja wa Taifa jijini Dar es Salaam (sasa Uhuru) na ulikuwa ni wa mzunguko wa pili Ligi Kuu Tanzania Bara.

Mchezo ulianza kwa kasi, huku timu zote zikishambuliana kwa zamu. Yanga walikuwa wanashambulia na pindi Simba nao walipokuwa wanapata nafasi walikuwa wanashambulia pia.

Mabeki wa timu zote mbili walikuwa makini mno katika kudhibiti mashambulizi yaliyokuwa yakielekezwa langoni mwao, huku washambuliaji nao walikuwa wakifanya mashambulizi kadhaa wakiwa na lengo la kutaka kupata bao la mapema mapema.

Mashambulizi ya Yanga, yalikuwa yakiongozwa na Davies Mwape, Kenneth Assamoah na Amisi Kiza, huku mashambulizi ya Simba yalikuwa yakiongozwa na Felix Sunzu, Emmanuel Okwi na Ulimboka Mwakingwe.

Kosa kosa za kutaka kufunga zilikuwa zikitokea pande zote mbili, kwa sababu mabeki walionekana kuwa imara katika kudhibiti mashambulizi ya washambuliaji.

Katika dakika ya 30 hivi, Simba walifanya shambulizi moja kali langoni mwa timu ya Yanga, lakini shuti hafifu alilopiga Emmanuel Okwi, lilidakwa kirahisi na kipa wa Yanga Yaw Berko.

Yanga ilijibu shambulizi hilo katika dakika ya 32 hivi, baada ya kiungo wao mahiri Haruna Niyonzima kutoa pasi kwa Kenneth Assamoah, lakini shuti lake lilitoka sentimita chache langoni mwa timu ya Simba.

Dakika ya 40 hivi, Simba walifanya shambulio lingine kali langoni mwa timu ya Yanga, lakini Sunzu aliyecheza vizuri siku hiyo, alikosa bao la wazi baada ya kubaki yeye na kipa wa Yanga Berko, kwani shuti lake kali alilopiga lilitoka nje kabisa.

Hadi dakika 45 za kipindi cha kwanza zinamalizika, timu hizo zilikwenda mapumziko matokeo yakiwa ni suluhu ya 0-0.

Kipindi cha pili nacho kilianza kwa kasi, huku timu zote mbili zikifanya mabadiliko ya wachezaji wao. Katika dakika ya 50, Simba ilimpumzisha Amri Kiemba na nafasi yake kuchukuliwa na Haruna Moshi 'Boban'.

Kuingia kwa kiungo mashambuliaji 'Boban', kwa kiasi fulani kuliongeza kasi ya mashambulizi kwa upande wa Simba, kwani walionekana kufanya mashambulizi mengi langoni mwa timu ya Yanga tofauti na mwanzoni.

Yanga kwa kutaka kuongeza mashambulizi mbele, katika dakika ya 55, ilimtoa Amis Kiza na nafasi yake kuchukuliwa na Idrisa Rashid ambaye baada ya kuingia alioneza kasi ya mashambulizi kwa timu yake ya Yanga.

Dakika ya 70 hivi, Simba ilimtoa winga wa kushoto Ulimboka Mwakingwe na nafasi yake kuchukulia na Mwinyi Kazimoto.


Katika dakika ya 75 hivi, Yanga walifanya shambulio moja la nguvu langoni mwa timu ya Simba na kufanikiwa kupata bao la kuongoza ambalo lilifungwa na Davies Mwape.

Dakika ya 80 hivi, Yanga ilifanya badiliko lingine kwa kuingia Jerry Tegete aliyechukua nafasi ya mfungaji wa bao pekee Davies Mwape.

Pamoja na mabadiliko ya wachezaji kufanywa na pande zote, lakini hapakuwa na mabadiliko ya matokeo, hivyo hadi dakika 90 za mchezo zinamalizika, Yanga walitoka uwanjani wakiwa vifua mbele baada ya kumfunga mtani wake wa jadi Simba bao 1-0.

Kikosi cha Yanga: Yawa Berko, Godfrey Taita, Oscar Joshua, Chacha Marwa, Nadir Haroub 'Cannavaro', Juma Seif 'Kijiko', Nurdin Bakari, Haruna Niyonzima, Davis Mwape/Jerry Tegete, Kenneth Assamoah na Amis Kiza/Idrisa Rashid.

Kikosi cha Simba: Juma Kaseja, Said Nassor 'Chollo', Juma Jabu, Juma Nyoso, Victor Costa 'Nyumba', Jerry Santo, Amri Kiemba/Haruna Moshi 'Boban', Shomari Kapombe, Felex Sunzu, Emmanuel Okwi na Ulimboka Mwakingwe/Mwinyi Kazimoto.



JAMVI LA HABARI
SPOTI
JUMATANO FEBRUARI 05, 2025



## Diamond afunguka kuhusu Mbosso

>> Soma Uk. 15

# YANGA, KEN GOLD NI VITA YA KISASI




NA MWANDISHI WETU

KIKOSI cha Yanga leo kitajitupa katika Uwanja wa KMC Kinondoni kuikabili timu ya Ken Gold iliyofanyiwa maboresho makubwa katika kikosi chake, katika kipindi cha usajili wa dirisha dogo.

Timu hiyo iliyoyumba sana katika mzunguko wa kwanza Ligi Kuu NBC, itaikabili Yanga baada ya kusajili idadi kubwa ya wachezaji, wengi wakiwa ni wazoefu akiwemo kiungo mshambuliaji aliyewahi kutesa akiwa na Yanga Benard Morrison.

Usajili mzima wa kikosi hicho chenye maskani yake katika Jiji la Mbeya ni Bernard Morrison, Obrey Chirwa, Erick Kabamba, Fredrick Kalubunga pamoja na Kelvin Yondani beki mkongwe aliyewahi kuchezea timu za Simba na Yanga.

Wengine ni Zawadi Mauya, Emmanuel Asante, Mubashid Seidu, Kyala Lassa, Elnest Kwofie, Thompson Unachi, Mohamed Yusuph, Mathias Juviliani, Abdul Abdulai, Maulid Mbegu, Sele Bwenzi, Joseph Ambokege, Ahmed Chambela, Sadala Lipangile, Sandale Komanje na Rojas Gabriel ambao wengi kati yao wanatarajiwa kuonekana uwanjani hii leo.

Wakati wababe hao wa mjini Mbeya wakijinasibu kushinda mechi ya kesho naye kocha wa Yanga Sead Ramovic, amesema timu yake itaingia katika mechi hiyo ikiwa na tahadhali zote ili kuhakikisha wanapata ushindi.

# Rekodi ya Camara Simba usipime

NA MWANDISHI WETU

KIPA wa Simba Mousa camara ameendelea kujjizolea sifa tangu alipojiunga na Klabu hiyo msimu uliopita, hivi sasa akiweka rekodi ya kuvutia katika mechi zlizokwishaichezea timu hiy tangu alipojiunga nayo akitokea Horoya FC ya nchini Guinea.

Camara aaliyefanikiwa kuondoa Ufalme wa kipa mkongwe nchini Aishi Manula katika kikosi cha Simba hadi sasa ameshaichezea timu hiyo yenye makao yake Msimbazi Jijini dar es salaam mechi 16.

Katika mechi hizo kwa mujibu wa takwimu mbalimbali, kioa



huyo alicheza kwa muda wa dakika 1440, akisaidia kuokoa mipira tisa ya hatari na kucheza mechi 13 bila kuurhusu bao langoni mwake.

Kutokana na msaada huo ndani ya kikosi cha Wekundu hao wa Msimbazi camare ameendelea kujizolea umaarufu pamoja na kuwa kipenzi cha mashabiki wengi, ambapo juzi alikuwa gumzo wakati timu hiyo ilipotinga Jijini Dodoma ambako imeweka kambi kwa ajili ya michuano ya Kombe la Shirikisho.

Timu yake hiyo inatatrajia kutupa karata yake katika michuano hiyo hatua ya Robo fainali, huku uongozi ukiweka dhamira ya kuhakikisha inavunja rekodi kwa kulitwaa Kombe hilo msimu huu.



## DAVIES MWAPE ALIPELEKA MAJONZI MSIMBAZI 2011

MIONGONI mwa matukio yaliyowahi kuwafurahisha wanachama na wapenzi wa klabu ya Yanga, moja ni lile la timu yao yenye maskani yake makuu Kariakoo, makutano ya mitaa ya Jangwani na Twiga, kumfunga mtani.

>> Inaendelea Uk. 15

GAZETI HILI HUTOLEWA NA JAMVI MEDIA GROUP, S. L. P 78862, DAR ES SALAAM